**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**06 STADI ZA KAZI, HAIBA NA MICHEZO**

**Muda: Saa 1:30** **Mwaka: 2015**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu mbili; A na B zenye jumla ya maswali **ishirini na tano (25)**
2. Jibu maswali **yote**

## SEHEMU A: Stadi za Kazi

Jibu swali la 1-7 kwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguzi nne ulizopewa na kuandika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku ulichopewa.

1. Aina mbili za unamu ni
   A mwembamba na mnene
   B mzito na mwepesi
   C mdogo na mkubwa
   D kwaruzi na mwororo.

2. Usafi na usalama ni kanuni kuu katika
   A upakuaji wa vyakula
   B upishi wa vyakula
   C ulaji wa vyakula
   D uzalishaji wa vyakula.

3. Mara baada ya kuchukua vipimo, mshonaji wa nguo anatakiwa
   A kuchora vipimo katika vigezo
   B kuandaa meza ya ushoni
   C kushona vigezo
   D kukata vigezo.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

4. ____________ huboresha sauti wakati wa kuimba.
   A Beti
   B Redio
   C Gitaa
   D Kinasa sauti.

5. Tunatumbukiza kindu kwenye maji ili
   A kuzisafisha
   B kuzilainisha
   C kuzifanya ziwe ndefu
   D kuongeza rangi

6. Kengele, pembe, tarumbeta na filimbi ni ala zinazotumika kucheza
   A majigambo
   B shairi
   C ngoma za asili
   D ngonjera

7. Tunafua nguo ili
   A kuondoa uchafu
   B kuongeza harufu nzuri
   C kuondoa rangi
   D kuongeza mng'aro.

Jibu swali la (8)-(12) kwa kuoanisha maelezo ya mbogamboga katika **Fungu A** na maelezo katika **Fungu B.** Andika herufi ya jibu sahihi katika mabano uliyopewa.

| | **Fungu A** | **Herufi** | **Fungu B** |
|---|---|---|---|
| 8. | Mboga za aina ya matunda | ( ) | A Spinachi |
| 9. | Mboga za aina ya miziz | ( ) | B Vitunguu saum |
| 10. | Mboga za aina ya majani | ( ) | C Viazi mviringo |
| 11. | Mboga za aina ya maua | ( ) | D Njegere |
| 12. | Mboga za aina ya mbegu | ( ) | E Nyanya |
| | | | F Koliflawa |
| | | | G Karoti |

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Jibu swali la 13-15 kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

13. Faida ya kufuga kuku wa kienyeji ni kupata nyama na _________ ambavyo ni vyanzo vya protini.

14. Vitambaa vya meza hurembwa kwa kutumia mishono ya________________

15. Aina ya upishi inayotumika kutengeneza mikate huitwa_________________

**SEHEMU B: HAIBA NA MICHEZO.**

Jibu swali 16-22 kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kisha kuiandika kwenye kisanduku ulichopewa.

16. Watu hufanya mawasiliano ili
   A kuwapatia watu wengine taarifa
   B kusalimiana na watu kwa kuongea
   C kujenga moyo wa kufanya kazi kwa pamoja
   D kuvitumia vifaa vya mawasiliano.

17. Faida ya ubunifu ni
   A uumbaji wa vifaa mbalimbali
   B kukuza vipaji vya watu
   C kujishughulisha katika kazi
   D kuweza kununua vifaa vya ubunifu.

18. Riadha ni mchezo unaojumuisha
   A mbio fupi na mbio ndefu
   B kutupa tufe na kisahani
   C kuruka chini na kuruka juu
   D mbio, miruko na mitupo.

19. Njia ya kukabili mienendo hatarishi ni pamoja na
   A kupita chini ya nyaya za umeme
   B kuvaa viatu
   C kucheza barabarani
   D kucheza katika majalala ya taka.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

20. Tendo linaloonesha uamuzi wa busara ni
A kuomba ushauri kabla ya kuamua
B kuomba ushauri baada ya kuamua
C kuomba ushauri wakati wa kuamua
D kufuata uamuzi wa watu wengi.

21. Faida ya kulinda na kutunza mwili ni
A kuwa na mafuta mengi mwilini
B kuwa na utulivu wa akili
C kuwa na virutubisho vya ziada mwilini
D kuzuia kifo.

22. Vipindi viwili vya mchezo wa mpira wa miguu vina jumla ya
A dakika 70
B dakika 45
C dakika 80
D dakika 90.

Jibu swali la 23-25 kwa kujaza sehemu zilizoachwa wazi.

23. Mchezo unaohusisha kujisawazisha, kujitoma, na kujifyatua unaitwa ________

24. Mchezo wa rede huchezwa kwa kutumia ________________________________

25. Hali ya kujali na kuheshimu watu hujulikana kama _______________________

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org